BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Pili – Tarehe 14 Septemba, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

81. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu kwa Kwanza wa Rais:

    Kwa kuwa Zanzibar imezungukwa na bahari na kutokana na ongezeko la mmong'onyoko wa ardhi, sehemu nyingi zilizo karibu na bahari zinaathirika na hali hiyo.

    Je, ni mkakati gani wa Serikali unaofanyika kudhibiti hali hiyo.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

17. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Kutokana na ujenzi holela na usiofuata mipango miji, wananchi wa jimbo la Nungwi wanaendelea kupata madhara mbali mbali hasa kutokana na ajali za moto zinazotokea kila siku hasa mahotelini.

    (a) Je, kikosi chetu cha Zimamoto na Uokozi, kimejipanga vipi katika kuzikabili ajali hizo katika jimbo la Nungwi na sehemu nyengine zilizojengwa bila ya kufuata Mipango Miji.

    (b) Je, Wizara ikishirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokozi ina mpango gani juu kuongeza visima vya 'FIRE HYDRANT" kwenye maeneo ya mahoteli na hata kwenye nyumba za vijijini.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

94. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Serikali hapo awali ilizielekeza Halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa makundi maalum, yaani wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kiwango cha 4-4-2. Kwa kuwa jambo hili kwa sasa limehamishiwa kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

(a) Je, mgao huu unayazingatia vipi makundi hayo maalum yaliyotambuliwa hapo awali.

(b) Je, ni kwa kiasi gani mgao huu unazingatiwa huko kwa Wakala wa Uwezeshaji.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

43. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kituo cha Elimu na Sanaa kilichopo Mwanakwerekwe kinaweza kuwa na mchango mkubwa wa kuziba pengo la ajira katika kuwawezesha wananchi kujiajiri wenyewe.

Je, ni lini hasa Serikali itafanya maamuzi sahihi ya kukiwezesha kituo hiki ili kitimize malengo yaliyokusudiwa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

2. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwa kawaida baadhi ya Wizara, Idara au Taasisi za Serikali zinapokuwa na shughuli nyingi za kiofisi au za Kiserikali zikiwemo ziara za viongozi wakuu wa nchi, huomba msaada wa kupatiwa vyombo vya moto kama vile gari katika mashirika na taasisi zinazojitegemea kama vile ZSSF kwa lengo la kufanikisha shughuli hizo. Changamoto inayojitokeza baadae ni kuwa taasisi hizo za Serikali zinashidwa kurudisha gari hizo baada ya shughuli zao kuisha, jambo ambalo linarudisha nyuma utendaji kazi wa mashirika na taasisi hizo zinazojitegemea kwa kutozitumia gari hizo katika shughuli zao.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuja na mfumo mzuri utakaondoa malalamiko yanayotokana na taasisi moja kuazima gari kwa taasisi nyengine ya Serikali bila ya kuirudisha kwa wakati au kutoirudisha kabisa.

(b) Je, lini magari yaliyoazimwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na taasisi mbali mbali za Serikali yatarudishwa licha ya kuwa mfuko huu umeshachukua jitahada kadhaa za kuomba kupatiwa gari hizo lakini bado hazirudi katika himaya yao.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyombo vya moto kama vile gari katika taasisi zake kwa lengo la kupunguza changamoto ya ukosefu wa vyombo hivyo jambo linalopelekea shughuli mbali mbali za kiserikali kuzorota na kukosa ufanisi.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

55. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wizara ya Afya imeunda Baraza la Tiba Asili kwa ajili ya kuwasajili na kuwatambua wanaohusika na kutoa tiba mbali mbali mbadala hapa nchini.

(a) Je, ni utaratibu na vigezo gani ambavyo vinatumika kuwasajili waganga wa Tiba Asili.

(b) Je, katika kuwasajili waganga hao wa Tiba Asili, ni kiasi gani cha gharama kinachotumika kulipia usajili huo.

56. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni tafiti gani ambazo zimefanywa kutoka katika maabara zetu za afya ya jamii na kuleta matokeo chanya kwa miaka ya hivi karibuni.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

29. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, kuna aina ngapi za wadudu waharibifu wa mazao mbali mbali ya kilimo ambao katika ukuaji wao wanaathiri na kudumaza uzalishaji wa mazao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

16. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaipongeza Serikali kwa kupatikana huduma bora ya umeme Unguja na Pemba. Hata hivyo, changamoto ya kuwepo kwa umeme mdogo katika kisiwa cha Pemba, inaendelea kuikabili Wizara yako, hali inayopelekea kuharibika kwa vifaa vya umeme vya wananchi lakini hata vya taasisi zetu za Serikali.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea tatizo hilo.

(b) Je, ni upi mkakati na mipango ya Wizara yako kuhusika na tatizo hili.

(c) Kwa kuwa kumekuwa na hospitali kubwa za Wilaya na Mkoa ambapo vifaa vingi vipya vimeingizwa. Na kwa kuwa huduma ya upasuaji inategemea umeme wa kutosha, Je, kwa upande wa hospitali, Wizara yako inaliangalia vipi tatizo hili la umeme mdogo unaosababisha athari kubwa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**14 Septemba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**